

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA AROBAINI NA TISA**

**10 JUNI, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA TISA – TAREHE 10 JUNI, 2021

#### I. DUA:

#### II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

##### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mipango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

#### III. MASWALI:

##### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

##### 405. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kituo cha Afya Msindo kilichopo Wilayani Namtumbo kinapata mgao mdogo wa Dawa usiokidhi mahitaji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mgao wa Dawa katika Kituo hicho.

**406. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaajiri Walimu wa Masomo ya Sayansi katika Shule za Sekondari za Halmashauri ya Mji wa Mbulu ili Wanafunzi wapate ujuzi wa masuala ya Sayansi.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**407. MHESHIMIWA ALLY YAHYA MHATA (NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Wananchi wa Jimbo la Nanyumbu wananufaika vipi na Ranchi ya Nangaramo.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **408. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia Wananchi wa Mbagala Kokoto hadi Kongowe wanaopisha ujenzi wa Barabara ya Kilwa.

## **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

### **409. MHESHIMIWA ALI HASSAN OMAR KING (JANG'OMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua Ofisi Ndogo ya Hazina Zanzibar kama ilivyo kwa Taasisi nyingine za Muungano ili kurahisisha huduma kwa Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wanaoishi Zanzibar.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**


Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

##### **SAA 10:00 ALASIRI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.



**DODOMA**  
**10 JUNI, 2021**



**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**